# WOKOVU KATIKA DHAMBI WAWEZAJE KUPATIKANA?

Na

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian
Masihi Mau'udi

ISLAM INTERNATIONAL PUBLICATIONS LTD

# Wokovu katika Dhambi Wawezaje Kupatikana?

**Tafsiri ya Kiswahili ya:**
Ghunah Se Najaat Kiyunkar Mil Sakti Hai? (Kiurdu)
Ghunah Se Najaat Kiyunkar Mil Sakti Hai? (Swahili Translation)

**Mwandishi**
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian

**Mfasiri**

Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani

Chapa ya Kwanza (Kiurdu): 1902
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): 2022

© Islam International Publications Ltd.

**Kwa Maelezo Zaidi:**

**Tanzania:**
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dar es Salaam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744

**Kenya:**
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi Kenya Simu: +254222111031

Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salaam, Tanzania / Nairobi, Kenya

Cover design by Ibrahim Ijaz

**ISBN:**
978-1-84880-517-0
10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

# MAELEZO YA MWENEZI

Kitabu hiki kilicho mikononi mwenu ni tafsiri ya makala ya Mwanzilishi Mtukufu[as] wa Jumuiya ya Waislamu Waahamadiyya, yaliyochapishwa katika *The Review of Religions* (Kiurdu) ndani ya toleo lake la Januari 1902, na tafsiri yake ilitolewa katika *The Review of Religions* (Kiingereza) ndani ya toleo pia la Januari 1902.

Hadhrat Khalifatul Masihi V[atba] aliagiza kuyaingiza ndani ya Ruuhaani Khazaain (Jalada la 18).

Kitabu hiki kimeeleza tofauti ya fikara ya Islam na dini nyinginezo, hususan Ukristo. Islam yakataa katakata wazo la dhambi ya asili; yafundisha kwamba kila mtu ataadhibiwa kwa dhambi zake wala si kwa dhambi za mwingine. Seyidna Ahmad[as] ametoa majibu ya kutosha kuhusiana na maswali yote ya muhimu kuhusu habari hii.

Mwanzilishi mtukufu[as] amefanya malinganisho kwa marefu na mapana baina na mafundisho ya Islam na dini nyinginezo kuhusu wokovu, na amehakikisha kwamba Islam pekee ndiyo dini iwezayo kumwongoza mtu kwenye utambuzi kamili wa Mungu na hatimaye kumjaalia kuepukana na dhambi na kupata wokovu wa kweli.

Kitabu hiki kimefasiriwa na Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani, kisha nikaidurusu na kuilinganisha na matini ya Kiurdu. Sheikh Ansar Hussain akazipanga herufi zake kwa kompyuta na kutayarisha fomati.

Mwenyezi Mungu Awabariki wote waliohusiana na kazi hii ya muhimu na Awajalie wasomaji wanufaike nayo kiroho, kielimu na kimatendo.

Jamil R. Rafiq

Wakilut-Tasnif
Tahrike Jadid
Rabwah, Pakistan. 27 Machi 2021

## WOKOVU KATIKA DHAMBI WAWEZAJE KUPATIKANA?

Katika kitabu hiki tunanuia kuionyesha dunia ya kuwa kiasi zama zetu hizi zilichoshastawi kimwili, kiasi hicho hicho zimerudi nyuma kiroho hata kwamba roho hazistahimili kuweza kuzikaribia kweli takatifu. Bali kwa kuwatazama wanadamu kwa makini inathibitika kwamba kivutio kikubwa ndani kwa ndani kinawavuta upande wa chini, nao kila wakati wanaelekea kwenye shimo ambalo twaweza kusema, kwa maneno mengine, hali ya chini kabisa kuliko ya wale walio chini. Na katika vipawa yametokea mapinduzi ya namna hii kwamba wanavisifu sana vitu ambavyo kwa mtazamo wa kiroho vinachukiza na ni vibaya. Dhamira ya kila mmoja inahisi kwamba kivutio fulani kinamwelekeza chini, na kwa athari za kuangamiza za vivutio hivyo, ulimwengu mzima umeangamia. Kweli takatifu zinatazamwa kwa dhihaka na masihara, na kuelekea kwa Mungu kunachukuliwa kuwa ujinga hasa. Nafsi zote zilizopo ardhini zinaonekana kuangukia kabisa katika dunia, kana kwamba wameshindwa na kulazimishwa na nguvu iliyofichamana ya kuvutia. Hili ni jambo ambalo tumeshaliandika mapema kwamba shughuli zote za dunia zinategemea vivutio. Jiha yenye nguvu zaidi ya yakini inavutia kwake jiha nyingine. Kwa vile falsafa hii ni sahihi kabisa kwamba kivutio kimoja kinaweza kuzuiliwa na kivutio kile tu ambacho kina nguvu zaidi kuliko hicho, kwa hiyo dunia hii ambayo ikiathirika na

kivutio cha chini inavutika upande wa chini, kuigeuza iende upande wa juu haitegemewi kabisa mpaka kivutio kingine kilicho kinyume chake na chenye nguvu zaidi kizalike toka mbinguni ambacho kiongeze yakini ya jiha iliyo dhidi yake; yaani, kiasi zinachohisika, kwa mtazamo wa yakini, faida na ladha katika vitendo vibaya vya nafsi, zaidi kuliko hizo zionekane faida katika amri za Rahmani, na kwa mtazamo wa yakini kitendo cha maovu kionekane sawa sawa na mauti, kinachoumiza moyo. Na mwanga huu wa yakini unakuja toka mbinguni kupitia jua lile lililo Imamu wa zama. Kwa hiyo, kutomtambua Imamu yule ni kufa kifo cha ujahili. Mtu anayesema sitaki kupata mwanga wa jua hilo, anataka kuvunja kanuni ya kudumu ya Mungu. Je, yawezekana macho kuona bila jua? Ingawa machoni pia mna nuru fulani, lakini hulihitaji jua. Jua ni nuru ya kweli inayokuja kutoka mbinguni na inaing'arisha ardhi, na macho bila hiyo ni kipofu. Na yule mtu atakayezalikiwa na yakini kwa nuru hiyo ya kimbingu, atavutika kwenye wema. Na kuvutana baina ya kivutio cha kimbingu na kivutio cha kiardhi ni jambo la kawaida. Kwani, katika hali hiyo kivutio kimoja kitavuta kwenye wema na kingine kwenye uovu; kimoja kitasukuma upande wa mashariki na kingine upande wa magharibi. Na itakuwa hatari hivyo viwili kugongana wakati vyote viwili vitakapokuwa na vivutio vya hali ya juu, ambavyo kutopatikana kwavyo ni jambo la lazima wakati wa maendelezo ya juu ya dunia. Basi, muonapo

ardhi imeishapata maendeleo ya hali ya juu, muelewe kwamba siku hizo ni za maendeleo ya kimbingu pia. Na muwe na yakini kwamba kuna matayarisho ya kiroho huko mbinguni pia na huko pia kivutio fulani kimezalika kinachotaka kupigana na kivutio cha ardhi, basi siku za namna hii ni za hatari sana ambamo ardhi izidi sana mno katika mghafala  na uovu. Kwani kwa vita vya kiroho, siku za ahadi ni zile zile zilizoelezwa na manabii katika istiara za namna mbalimbali. Na baadhi yao wameeleza habari hii katika methali hii kwamba hii ni vita ya mwisho kati ya malaika wa mbinguni na mashetani wa ardhini ambapo dunia hii itakwisha. Na baadhi yao kwa ujahili na ujinga wao, wameyachukulia mapambano hayo kama vita ya kidhahiri inayopiganwa kwa upanga na bunduki. Lakini watu hao wamekosea, na kwa akili yao mbovu na ujahili wameichukulia kwa nguvu vita ya kiroho kuwa vita ya kimwili. Ilmuradi, siku hizi kuna vita vya mwisho kati ya giza la ardhi na nuru ya mbingu. Tangu Adamu mpaka Nabii wetu[saw], manabii wote watakatifu wa Mungu waliendelea kuashiria kwenye vita hivyo. Na Makamanda wa vita hivyo wameitwa majina mawili tofauti; mmoja mwenye kuzificha kweli na wa pili mwenye kuzidhihirisha kweli; au kwa maneno mengine imeelezwa kwamba mshukaji kutoka mbinguni pamoja na Malaika wa nuru na dhihirisho la Mikaeli, na mwingine mwenye kudhihirika toka ardhi akiwa na magiza yote ya kishetani, na atakuwa dhihirisho la Iblisi. Sasa tunapoona kwamba

jeshi la ardhi limeshajiandaa sana na limesimama kwa kushika silaha na kufanya kazi yake, bali limeshaifanya kiasi kikubwa, hapo kikawaida huzalika hamu njema, na busara sahihi inashuhudia kwamba serikali ya kimbingu pia haikuyafumbia macho matayarisho hayo. Serikali hii ina tabia ya namna hii kwamba haipendi makelele ya kidhahiri, na inafanya mambo mengi ndani kwa ndani bila watu kupata habari. Ndipo hudhihirika ishara moja mbinguni na mnara ung'aao na mweupe sana ardhini, na mwanga ule wa mbinguni unauangukia mnara, kisha mnara ule unang'arisha dunia nzima. Sentensi hii ndogo inahitaji maelezo. Na maelezo yake ni haya kwamba ingawa nidhamu ya kiroho ya Mwenyezi Mungu inaafikiana kabisa na nidhamu ya kimwili, lakini katika baadhi ya mambo kuna sifa za ajabu ndani yake ambazo haziwezi kuonekana waziwazi katika nidhamu ya kimwili. Miongoni mwa sifa hizo, sifa mojawapo ni hii pia kwamba kivutio cha dunia kinapoanza kufanya kazi yake, basi ingawa kivutio kile ni kinyume kabisa cha kivutio cha kimbingu, hata hivyo kivutio cha kimbingu huanza kuzalika kwa sababu ya matakwa ya asili ya kivutio kile. Basi jambo hili ni la akili kwamba wakati wa nguvu za hali ya juu za vivutio hivyo, ulio zama za mwisho za dunia, ilipaswa vita ipiganwe baina ya hivyo viwili. Kwani, utashi wa nguvu ni kuangamiza kundi lililo adui. Basi makundi mawili yatakapokuwa na nguvu na hadhi ya kiwango kimoja, makundi mawili ya namna hii hayana budi kupigana, kwani kila kimoja [katika

vivutio hivi viwili] kimeelezwa kama bishara katika vitabu vya manabii wa Mungu. Kadhalika akili pia inafikiria jambo hili kuwa la lazima, kwani vivutio viwili vyenye nguvu vinavyohitilafiana vitakapogongana, basi ni lazima kimoja kiangamize cha pili, au vyote viwili viangamie. Kuhusiana na mapambano hayo imeelezwa katika vitabu vya manabii hivi kwamba miaka elfu kamili ilipopita tangu Hadhrat Masihi[as] ambamo, sawa na bishara ya manabii, shetani alikuwa amefungwa, hapo kivutio cha uovu kilianza kuimarisha athari yake ardhini. Hizo zilikuwa ni zama Islam ilipoanza kuelekea kurudi nyuma katika kushikamana na mafundisho yake matakatifu, na maendeleo yake ya kiroho yakazuilika, na mfululizo wa ushindi wake wa kidhahiri pia ukakoma. Na hali hii ilizalika katika zama za kufungwa kwa shetani. Na ililazimika kuwa hivyo kama ambavyo manabii wote mpaka Yohana Fakihi walishuhudia. Na baada ya shetani kuachiliwa, yaani miaka 1000 baada ya Yesu, Islam ilianza kurudi nyuma na ikakoma kusonga mbele, ndipo harakati za shetani zilianzia kwa namna mbalimbali. Na mmea huu uliendelea kukua juu ya ardhi, na baadhi ya matawi yake yalienea upande wa mashariki na mengene yalifikia sehemu za mbali zilizokaliwa na watu upande wa magharibi, na mengine upande wa kusini na mengine yalielekea upande wa kaskazini. Kama vile zama za kumfunga shetani zilivyokuwa miaka elfu ambayo matukio ya dhahiri yalishuhudia, ndivyo zilivyokuwa zama za kuachiliwa

kwa shetani miaka elfu, zinazokamilika mwanzoni mwa karne ya kumi na nne Hijria. Lakini, miaka hiyo elfu moja ni sawa na hesabu ya Kiungu, yaani sawa na hesabu ya mwezi. Wayahudi na Waislamu wamefundishwa hesabu hii hii kutoka kwa Mungu kwa kutambua nyakati za bishara. Na njia ya kuhesabu sawa na siku za jua ilianzishwa na wanadmu iliyo kinyume cha matakwa ya maandiko matakatifu. Ilmuradi, sawa na hesabu hii, siku hizi tuliomo humu ni za mwisho za muhula aliopewa shetani, bali mfahamu kwamba zimeshapita pia, kwani karne ya Hijria ambayo mwanzoni mwake miaka elfu ya kuachiliwa kwa shetani ilitimia na imeishapita miaka kumi na tisa. Na shetani hataki anyanganywe uhuru na utawala wake. Lazima vita itatokea baina ya vivutio viwili iliyopangwa tangu mwanzo, na haiyamkiniki kwamba Neno la Mungu libatilike. Na juu ya siku hizi kuna ushahidi huu mwingine pia kwamba tangu mwanzo wa dunia, yaani tangu kudhihirika kwa Adamu mpaka leo, elfu ya sita pia imepita ambamo Adamu wa pili alipaswa kuzaliwa. Kwani siku ya sita ni siku ya kuzaliwa kwa Adamu. Na sawa na vitabu vitakatifu vya Mungu miaka elfu moja ni kama siku moja. Hivyo, hakuna budi kukubali sawa na ahadi takatifu za Mungu kwamba Adamu yule ameshazaliwa, ingawa bado hajatambuliwa kikamilifu. Na papa hapa twalazimika kukubali hii pia kwamba mahali pa Adamu palipopangwa kwa mkono wa Mungu ni Mashariki wala sio Magharibi, kwani inathibitika

kutokana na Torati[1], mlango wa 2, aya ya 8, hii tu kwamba Adamu alipewa mahali upande wa Mashariki katika busani moja. Kwa hiyo, ni lazima kwamba Adamu huyu pia adhihiri katika nchi ya Mashariki ili kushabihiana kwa mwanzo na mwisho kuhusiana na mahali kubaki. Na kukiri huku kama ambavyo Waislamu hawana budi, ndivyo Wakristo pia wasivyoweza kukataa sharti tabia ya ukanaji Mungu usiwe kikwazo. Basi kwa kuelewa uhakika haikubaki mishikili yoyote. Na jambo hili ni wazi kabisa kwamba zama hizi ni zama za mapambano kati ya mwanga na giza, na giza limeshamaliza kazi yake hadi mwisho, na haiwezi kutarajiwa kwamba bila kushuka nuru ya kimbingu, yeyote aweze kulishinda giza hili. Na hakuna shaka hata kidogo katika jambo hili kwamba giza limeshaimarika kikamilifu na taa ya ukweli iliyofifia sana imekaribia kutilifika, na itikadi rasmi, elimu rasmi na sala rasmi haziwezi kuurudisha kwenye hali ya awali mwanga huu ulioishapotea. Je, kipofu anaweza kumwongoza njia kipofu? La, hasha! Je, giza linaweza kuliondoa giza? Kamwe haiyamkiniki. Sasa unahitajika mnara mpya ambao utayarishwe juu ya ardhi ulio juu sana mno kuliko miji ya chini, ili nuru ya kimbingu iushukie, na taa ya kimbingu iwekwe juu yake, kisha dunia nzima imulikike kwa mwanga huu. Kwani kama taa isipowekwa mahali pa juu, itawezekanaje mwanga wake

[1] Mwanzo, 2:8 (Mwenezi)

uenee mpaka mbali. Sasa iliyobaki ni kwamba mfahamu mnara ni kitu gani. Kumbukeni, basi kwamba mnara ni jina la ile nafsi takatifu iliyotakata na yenye ushupavu anayopewa mtu kamili anayestahiki kupata nuru ya kimbingu, kama ambavyo matilaba hayo yamo katika maana ya mnara. Na muradi wa urefu wa mnara ni ushapavu wa hali ya juu wa mtu huyo. Na maana ya uimara wa mnara ni uimara wa mtu huyo anaoonyesha wakati wa mitihani ya aina aina, na hatimaye weupe wake na utakaso wake unadhihiri. Na hayo yote yanapoishafanyika – yaani wakati ambapo kwa bidii yake ya hali ya juu, uimara wake kamili, subira yake kamilifu, uthabiti wake na dalili zake, unabainika utakaso wake kama mnara ung'aao – ndipo unawadia wakati wa ujio wake wa jalali, na ujio wa kwanza uliokuwa na mitihani, muda wake unakwisha. Hapo hali ile ya kiroho ikipata sifa ya jalali ya Mungu inamshukia yule anayesimama kwa sura ya mnara, ndipo kwa idhini ya Yule Mtakatifu athari ya Kiungu zinazalika ndani yake. Hayo yote yanatokea katika ujio wa pili. Na ujio hasa wa Masihi Mau'udi ni picha kamili ya uhakika huo. Na masimulizi haya yaliyopo baina ya Waislamu kwamba Masihi Mau'udi atashuka karibu na mnara, hapo maana ya kushuka ni ujio wa kijalai ambao unayo sifa ya Kiungu. Sio kwamba yeye hakuwepo ardhini hapo kabla, lakini hakuna budi mbingu iwe naye mpaka wakati ule uwadie Alioupanga Mungu. Katika suna ya Mungu imo hii pia kwamba kwa kufahamisha mambo

ya kiroho Anaweka picha pia ya kimwili ya sehemu yake fulani kama vile Hekalu la Baitul Makdis na Kaaba ya mji mtakatifu Makka; hizo mbili ni taswira za madhihirisho ya kiroho. Kwa sababu hii hii imefahamika katika sheria ya Kiislamu kwamba Masihi Mau'udi atashuka juu ya mnara au karibu na mnara, katika nchi iliyopo upande wa Mashariki ya Dimashki – Damascus – kama vile Adamu pia alivyosakinishwa upande wa Mashariki. Kabla ya ujio huu wa kijalali haidhuru kujenga mnara wa kidhahiri pia, bali umetajwa katika Hadithi kama bishara kwamba kwa ujio wa kijalali wa Masihi Mau'udi, huo utakuwa alama moja, utakaojengwa kabla ya ujio wake. Hii ndiyo takdiri kwamba ujio wa Maishi Mau'udi utakuwa wa aina mbili; kwanza ujio wa kawaida ambamo mitihani ya aina aina imejaa, ni kipindi cha taabu mbalimbali. Siku hizo zitakapotimia ndipo kipindi cha ujio wa kijalali kitawadia. Na ni lazima kwamba kabla yake mnara mmoja uwe umetayarishwa kama vile ilivyotajwa katika Hadithi kwamba kwa kuonyesha uhakika huu, mnara wa kidhahiri pia utakuwepo, nao utakuwa taswira ya mnara wa kibatini. Na kabla ya kuteremka kwake kijalali, dunia haimtambui, kwani yeye hatokani na dunia, na dunia haimpendi, kwani Yule Mungu Ambaye yeye ametumwa naye, dunia haimpendi Yeye pia. Basi ni lazima ateswe katika ujio wa kwanza na audhiwe na atuhumiwe tuhuma za aina aina kama vile ilivyoandikwa katika matabiri ya Kiislamu kwamba mwanzoni Masihi

Mau'udi hatakubaliwa, na chuki za watu wapumbavu zitazidi sana dhidi yake na shari zao zitafika kileleni, hata kwamba mtu mmoja akimshambulia kidhuluma atadhani ametenda kazi njema sana, na mwingine akimuudhi atafikiri amemridhisha Mungu kwa kitendo chake. Itaendelea kutendeka hivyo, na tetemeko la kila aina litamsibu na ataukabili msiba wa kila aina hata kwamba ndani mwake suna ya Mungu itatimia. Ndipo utawadia wakati wa ujio wake wa kijalali, na wenye mioyo yenye bidii watafumbuliwa macho na wataanza kutafakari ni jambo lipi hilo, na huyo ni kadhabu wa aina gani ambaye hatiishwi, na kwa nini anajaaliwa misaada ya Mungu, na sisi hatuijaaliwi. Hapo malaika wa Mungu atawashukia mioyoni mwao na kuwafahamisha kwamba je, ni lazima kutimia bishara za hadithi zenu na masimulizi yenu, zinazosababisha kuwazuieni; na je hayawezi baadhi ya masimulizi yawe yametungwa na kuwa ghalati na yenye shaka; haijuzu baadhi ya bishara zitimie kiistiara? Je kulikuwa na sababu nyingine ya bahati mbaya na kutoamini kwa Wayahudi minghairi ya hii kwamba waliendelea kungojea mambo yote yatimie kidhahiri na yote yafanyike sawa na matamanio yao, lakini yote hayo hayakufanyika. Basi kama hata sasa pia Yupo Mungu Yule Yule na suna yake ndiyo ile ile, kwa nini haijuzu kwamba nyinyi pia mmepatwa na jaribio lile lile. Ilmuradi, hatimaye mioyo ya wanadamu kiasili itaelekea kwenye fikira hizi hizi kama inavyoendelea kuwa hivyo tangu zamani. Lakini jambo hili si sahihi

kwamba kwa kueneza dini ya kweli na ukweli zama hizi ni za vita za kidhahiri, kwani upanga hauwezi kudhihirisha johari za ukweli, bali unazificha zaidi na kutia shaka. Watu wanaotamani mawazo ya namna hii sio marafiki wa Islam, bali ni maadui; na asili yao ni mbovu na katika hali ya chini; na wamevunjika moyo; na mioyo yao haina bashasha na mabongo yao yamepumbaa, na tabia zao zina giza, kwani wanawapatia wapinzani nafasi ya kuleta upinzani unaoweza kweli kuletwa. Kwani, sawa na kauli yao Islam inahitaji jihadi kwa maendeleo yake, na hii ni aibu kwa Islam. Kwani, dini ambayo inayo nguvu hii kwamba inaweza kuthibitisha kwa urahisi ukweli wake kwa hoja za akili au kwa ushahidi wa kutegemewa wa aina nyingine, au ishara za kimbingu, dini kama hii haina haja kabisa ikubalishe ukweli wake kwa karaha na kwa kitisho cha upanga. Lakini kama katika dini fulani haina sifa hii ya asili na inaondoa udhaifu wake kwa upanga, basi kwa dini ya aina hii kuwa ya uongo haina haja ya dalili yoyote, upanga wake wenyewe unatosha kwa kuikata.

Lakini ukinzani huu kwamba kama jihadi haijuzu sasa, basi kwa nini katika zama za awali za Islam upanga ulitumiwa, hili ni kosa la wapinzani wenyewe lililozalika kwa kutoelewa. Hawajui kwamba Islam hairuhusu karaha kabisa kwa kueneza dini. Tazameni, namna gani katazo limo katika Kurani inaposema لَآ اِكْرَاهَ فِي الدِّيْنِ[2] yaani

[2] Al-Bakara, 2:257

haipasi kulazimisha katika dini. Basi, kwa nini upanga uliinuliwa? Uhakika wake wenyewe ni huu kwamba wasiostaarabika wa Arabuni ambao walikosa adabu na utamaduni, wakawa maadui wakali wa Islam na Waislamu. Na ilipokamilishwa hoja juu yao kwa dalili zilizo wazi kuhusu Tauhidi na kweli za Kiislamu na wakafahamishwa vizuri kwamba wakiwa wanadamu kuabudu mawe ni kosa kabisa, kwani ni kinyume cha ubinadamu pia, hapo hawakuweza kujibu mambo hayo ya kiakili. Na kwa kushindwa kwao kujibu, watu wenye busara walielekea kwenye Islam, na ndugu alitengana na ndugu, baba alitengana na mwana, ndipo kwa kuhifadhi dini yao batili hawakuwaza tadbiri nyingine isipokuwa kwamba kwa kuwaadhibu vikali wawazuie watu wasisilimu. Basi katika mji Mtukufu wa Makka, Abu Jahli na wengineo, machifu wa Makka, walianza kutekeleza mbinu hii. Wasomaji wa historia ya zama za awali za Islam wanajua vizuri kwamba wapinzani walifanya dhuluma kiasi gani katika Makka na wangapi wasiokuwa na hatia waliuliwa kwa dhuluma; hata hivyo watu hawakuzuilika kusilimu. Kwani, hata mwenye akili ndogo pia alitambua kwamba kinyume cha waabudu masanamu, Islam inatumia mantiki na maelezo safi. Kwa vyovyote wasipofaulu kwa tadbiri hii, ilipangwa kwamba Mtume Mtukufu[saw] mwenyewe auawe. Lakini Mwenyezi Mungu Akimlinda Alimpeleka huko Madina. Hata hivyo, wakamsaka ili kumwua, na kwa vyovyote hawakutaka kuacha mwenendo wao. Basi, katika hali hii,

Islam ilikuwa na njia ipi isipokuwa kujitetea dhidi ya mashambulizi hayo na kuwaadhibu washambuliao bila sababu. Kwa neno zima, vita za Islam hazikuwa kwa kueneza dini, bali zilikuwa kwa kulinda uhai wa Waislamu. Je, akili yoyote timamu inaweza kukubali kwamba Islam ilishindwa kuthibitisha kiakili Umoja wa Mungu hata mbele ya waabuduo masanamu pia wasiostaarabika? Na je, yeyote mwenye akili anaweza kukubali kwamba washirikina waliokuwa wakiabudu mawe na vitu visivyo na uhai nao walizoea kuishi ndani ya uchafu wa aina aina, Islam ilishindwa kihoja hata mbele yao na kutaka kutumia upanga? Mungu Apisha mbali, mawazo haya siyo sahihi kamwe; na waliopinga Islam kwa ukinzani wa aina hii, wameficha uhakika kwa dhuluma kabisa.

Naam, hii ni kweli kwamba kama vile masheikh walivyopata sehemu katika dhuluma hii, ndivyo ambavyo mapadri nao pia hawakubaki nyuma kupata sehemu, na wakileta upinzani wa aina hii wamepenyeza sana maneno ya masheikh majahili katika vichwa vya watu wa kawaida, na wakadanganyika hivi kwamba masheikh wetu wanatoa fatwa ya jihadi, na mapadri ambao ni wenye elimu sana nao pia wanaleta upinzani huo, kwa hiyo imethibitika kwamba kwa kweli dini yetu inaruhusu jihadi. Sasa ni dhuluma kubwa ilioje hii kwamba kwa mashuhuda mawili tofauti Islam imepingwa vikali. Kama mapadri wasingalifuata njia hii, bali wangaliufuata ukweli na kusema kwamba masheikh

hao wanatoa fatwa ya ujinga na ujahili, waila katika mwanzo wa Islam hali iliyozalisha haja hiyo, sasa katika zama hizi hali ile haimo, hapo ingetarajiwa kwamba mawazo yenyewe ya jihadi yangeondoka duniani. Lakini jazba ilikuwa nyingi na fahamu finyu, hivyo hawakuelewa uhakika.

Naam, hii ni kweli kwamba Waarabu baada ya vitendo vingi vya uharibifu kwa sababu ya kumwaga damu nyingi bila haki walipostahili kuuawa machoni mwa Mwenyezi Mungu, ndipo amri hii pia ilitolewa kwamba hao wote wanapaswa kuuawa. Hata hivyo, wakiamini watasamehewa kupewa adhabu ya kuuawa. Pengine wapinzani wenye fahamu ndogo walidanganyika kwa amri hii. Hawajui kwamba hali hiyo sio ya karaha, bali ni msamaha kwa wale waliostahili kuuawa; hakuna ujinga zaidi kuliko huu kuifahamu kulazimisha. Watu hao walistahili kuuawa kwa sababu ya kuwa wauaji sio kwa kufuru yao. Na Mungu Mwingi wa rehema Alijua pia vizuri kwamba wameshaelewa sana ukweli wa Islam. Kwa hiyo, rehemu yake ilitaka kwamba wenye hatia waliostahili kuuawa wapewe nafasi moja ya kupata msamaha wa dhambi zao. Basi kwa hili pia imethibitika kwamba Islam haikukusudia kamwe kumwua yeyote, bali waliolazimika kuuawa kwa mauaji yao nao pia walileteewa njia ya msamaha. Katika zama zile Islam ilikabili kila mahala matatizo haya kwamba katika kila kaumu uadui ulikuwa umezidi kiasi hiki kwamba mtu yeyote wa kaumu yoyote aliposilimu, yeye aliuawa au

uhai wake ukawa hatarini sana, na maisha yakawa yenye usumbufu kwake. Basi, katika hali hiyo Islam ililazimika kupigana vita kwa kuimarisha amani. Katika zama zile za majaribio, Islam haikutaka vita kamwe isipokuwa katika hali hizo mbili. Na Islam haikukusudia kamwe ipigane vita kwa dini, lakini ikalazimishwa kupigana bila kutaka kabisa. Basi yote iliyoyafanya Islam, ilifanya kwa kujihifadhi, kujitawala na kujitetea. Kisha baadaye masheikh wasiojua waliingiza ndani ya suala hilo maana nyingine, nao waliona fahari katika ukatili wenye aibu. Lakini hii si kosa la Islam; hii ni kosa la akili za watu hao wanaoona damu ya wanadamu yenye thamani ndogo kuliko damu ya wanyama; na hawajashiba na damu bali kwa lengo hili hili wanamsubiri Mahdi mmwaga damu, kana kwamba wanataka kuyathibitishia mataifa yote kwamba Islam kwa kujieneza ilihitaji daima karaha na kutumia nguvu, ilihali humo hakuna ukweli hata kidogo hata sawa na chembe.

Nionavyo, baadhi ya masheikh wa zama hizi hawajaridhika na hali hii ya kurudi nyuma inayoikabili Islam, na wakisisitiza itikadi kama hizi wanataka kuipeleka Islam mpaka kwenye daraja ya chini kabisa. Lakini fahamuni kwa yakini kwamba Mungu Hakubali kwamba Islam ilengwe na lawama na tuhuma kama hizi. Kwa wapinzani wasiofahamu, jaribio hili tu latosha kwamba wameshikilia kwa nguvu mpaka sasa itikadi yao hii kwamba katika zama za awali, hata baadaye pia, Islam iliendelea kutumia upanga kwa kuongeza jumuiya

yake. Na sasa zama hizi na wakati huu ndio wa kuliondolea mbali kosa hili mioyoni, sio kwamba liimarishwe zaidi. Kama masheikh wa Islam wakiafikiana wasisitize jambo hili kuondoa mioyoni mwa Waislamu katili, bila shaka watalifanyia kaumu hisani kubwa. Na si hilo tu, bali kupitia kwao mzizi mmoja imara wa sifa za Islam utawadhihirikia watu, na chuki zote walizonazo wapinzani wa dini dhidi ya Islam kwa makosa yao zitaondoka, ndipo macho yao, yakiwa safi, haraka sana yatafaidika na chemchemi hii ya nuru. Ni dhahiri kwamba yeyote hawezi kumkaribia mtu katili; kila mtu anamwogopa; hususan watoto na wanawake wanatetemeka wakimwona, naye anaonekana kama majununi. Na mpinzani mwenye dini nyingine anahofia hata kukaa naye usiku isije akainuka usiku na kumuua ili kuwa *ghazi.* Kwani, kwa fikara ya kupata thawabu, baadhi ya watu wa mipakani wakiua bila haki wanadhani kwamba leo kwa kitendo chetu kimoja tu tumeshapata Pepo, na tumestahiki kupata neema zake zote. Basi, ni aibu kubwa ilioje hii kwamba kaumu nyingine hazioni amani kukaa katika ujirani wa Waislamu, na hawawezi katu kupata kutulia mioyoni mwao kwamba kaumu hii ikipata nafasi itaweza kututendea wema kidogo. Mara nyingi mifano ya namna hii inaonekana kwamba mtu wa kaumu nyingine anakutwa kwamba anaongopa na kutetemeka kwa sababu ya itikadi hii iliyofichika ya Waislamu.

Nimeshapata kuona tukio la aina hii, na labda ni tukio la 20 Novemba 1901 alipofika Mwingereza mmoja huku kwetu Qadian. Wakati huo watu wengi wa Jumuiya yetu walishajumuika, na mazungumzo huhusu dini yakaendelea. Yeye akaja na kasimama pembeni. Hapo alikaribishwa kwa huluka njema na akakalishwa pamoja nami. Ilijulikana yu mtalii Mwingereza aliyeishatembelea Arabuni pia na anataka kupiga picha za Jumuiya yetu. Hivyo basi, alisaidiwa katika kazi hiyo na kwa kumburudisha na kumfurahisha aliombwa akae nami kwa siku chache; lakini ikatambulika kwamba aliogopa na akaeleza kwamba nimeshaona Waislamu wengi ambao wanawaua Wakristo kikatili. Akaeleza habari chache za namna hii za Baghdad pia ambamo matukio ya aina hii yalitokea kwa dhuluma sana. Ndipo alifahamishwa kwa upole sana na hulka kwamba Jumuiya hii iitwayo dhehebu la Ahmadiyya inazichukia sana itikadi kama hizi na hatuwapendi kabisa watu kama hao. Na kuhusiana na haki za kibinadamu, kazi litakayofanya dhehebu hili ni kuzing'olea mbali fikara kama hizi katika Islam. Hapo ndipo moyo wake ukatulia na kwa furaha akawa nasi usiku mmoja.

Shabaha ya kueleza kisa hiki ni kwamba itikadi za namna hii za Waislamu, zilizo kinyume kabisa na ukweli, zimedhuru sana mataifa mengine na mioyoni mwao mmezalika dhana mbaya na chuki. Na kuhusiana na huruma ya kweli ya Waislamu, dhana zao njema zimeshapungua sana; na kama wanazo kidogo, basi ni

juu ya watu wale ambao hawaishi maisha ya kisheikh wala hawajali kufuata mafundisho ya Kiislamu. Basi maadamu dhana mbaya kiasi hiki imezidi kuhusu Waislamu waliyosababisha wenyewe kuizidisha, basi je kuna dhambi kubwa pia kuliko hii kwamba masheikh kama hao na wafuasi wao wamewanyima wengi kupata baraka za Kiislamu. Je, dini ya namna hii inaweza kutoka kwa Mungu ambayo haiwezi kuingiza mafundisho yake mioyoni bila kuonyesha mng'ao wa upanga. Dini ya kweli ndiyo ambayo kwa sifa yake binafsi na uwezo wake na kwa hoja zake madhubuti yenyewe ifanye kazi ya upanga, sio kwamba ihitaji upanga wa chuma.

Hayo ni maovu yanayohitaji wakati wote kwamba msuluhishi azaliwe. Tunapotafakari hali ya ndani ya Islam, basi ni hali ya kutisha, kana kwamba jua limepatwa na sehemu yake kubwa imeishakuwa nyeusi na iliyobaki ni kidogo sana. Hali za kivitendo za Waislamu ni duni sana. Baadhi ya Hadithi zimebuniwa zinazoathiri vibaya sana hali yao ya kihuluka na ni dhidi kabisa ya kanuni zilizowekwa na Mungu. Kwa mfano, kanuni ya Mungu iliweka haki za aina tatu kwa wanadamu kwamba wasimuue yeyote asiye na hatia; na wasiharibu heshima ya yeyote bila kosa; na wasichukue mali ya mtu bila haki. Lakini naona kwamba baadhi ya Waislamu wameshavunja amri zote hizi tatu. Wanamwua asiye na hatia wala hawaogopi. Masheikh wao wapumbavu wameshatoa fatwa pia za namna hii

kwamba wanawake wa mataifa mengine ambao wanawaita makafiri na wasio na dini inajuzu kuwatorosha kwa hila au kuwakamata na kisha kuwaoa. Na kadhalika ni sawa tu kuchukua mali ya makafiri kwa njia ya hiana na wizi, si dhambi hata kidogo. Sasa yafaa kutafakari kwamba dini ile iliyoharibika kiasi hiki kwamba ndani yake wapo masheikh watoao fatwa za namna hii pia, dini ile imo katika hali ya hatari gani! Wafuatao matamanio yao ya nafsi wametunga wenyewe fatwa hizi zote na wamewazushia uongo Mungu na Mtume. Dhambi hizi zote wanazotenda katili wapumbavu, adhabu yake yote ni juu yao. Hao ni mbwamwitu, lakini wanadhihiri katika mavazi ya kondoo na kudanganya. Ni sumu hao, lakini wanajionyesha kama ni kiuasumu. Hao wanaitakia vibaya sana Islam na mahuluku wa Mungu, na hawana kabisa rehema wala huruma mioyoni mwao, lakini wanajificha. Wanatoa mawaidha kwa ujanja na kunuia kupata matamanio yao ya nafsi. Wanakuja misikitini katika mavazi ya watawa, lakini tabia zao za kifasiki huwa zimefichika. Hii sio hali ya nchi moja tu, wala si ya mji mahususi, wala si ya dhehebu maalumu, bali katika ulimwengu wote wa Kiislamu kuna kundi la watu wanaoitwa masheikh na kuvaa majuba ya kisheikh, na iwezekanavyo wanajifanya sura zao kama za watu wa dini ili wafahamiwe kuwa watawa na watakatifu; lakini vitendo vyao vinashuhudia kwamba hao ni akina nani, na ni watu wa mienendo gani! Hawataki uenee utakaso

wa kweli na huruma halisi duniani, kwani humo wanaona hasara yao.

Ilmuradi, siku hizi Islam imepatwa na matatizo makubwa. Roho nyingi zimekufa, hazielekei hata kidogo kwenye wema. Watu hao wameshaachana mara moja na njia ya wastani. Kuna kundi moja kati yao wanaoabudu makaburi na kuyazunguka kama Kaaba. Na wanaziona roho za viongozi wao kuwa na uwezo wote na kufanya zipendavyo kana kwamba zimepewa mamlaka ya hayo yote kutoka kwa Mungu. Mtayakuta makao mengi ya warithi wa masufii yaliyo na kaburi pia; wanawafanya wafuasi wao kuyaabudu. Na kama mtu anawauliza karama, basi wanaeleza maelfu ya karama za yule aliyezikwa kaburini, lakini hawanao uthibitisho wa hata mojawapo. Kwao kiini cha Islam ni kuabudu makaburi, na wanawachukulia Waislamu wengine kwamba wameshapotea. Hili ni kundi lililoshika njia ya kuruka kiasi katika kuzidisha. Kinyume chao kuna kundi la watu waliopunguza, nao wamepita mipaka katika ukanushaji kiasi hiki kwamba achilia mbali uwalii, kwao unabii pia si chochote wala lolote. Wanakanusha kabisa miujiza na wanaicheka na kuifanyia mzaha. Na kuhusu wahyi wanaeleza kwamba huo ni fikara tu za moyoni mwa mwenye Kitabu, naye anao ustadi wa kurekebisha kwa kuboresha fikara kama hizo. Na bishara iliyo mbali na ufahamu wa kiakili na iliyo na habari ya ghaibu halisi ni muhali. Ilmuradi, kwao wahyi wowote haushuki kutoka kwa Mungu wala muujiza si kitu wala bishara

haina uhakika wowote. Na makaburi ya wafu ni rundo la udongo tu, ambayo hayana uhusiano wowote na roho. Na kufufuka kwa wafu ni visa vya zama za ujahili, na fikira ya maisha ya akhera ni wazimu; na busara yote ndiyo kwamba mjipatie vipaji vya kuchuma dunia, na watu wanaoshughulikia kutwa kucha mambo ya dunia muwafuate na muwe kama hao.

Kuzidisha kupita mipaka na kupunguza kupindukia huhusiana na masiala ya unabii na maisha ya Akhera, lakini zaidi ya hayo kuna kuongeza na kupunguza kupindukia katika mambo ya maisha ya Waislamu. Hakuna kushika hali ya wastani katika kauli wala amali; katika maadili wala ndoa na talaka wala kushikamana na mke, wala katika maafikiao; wala katika ghadhabu wala huruma; wala katika kisasi wala msamaha. Ilmuradi, katika kaumu hii kuna ghasia ya ajabu ya hali ya juu; hakuna kipeo cha ujahili wala mipaka ya upotevu. Basi kama kaumu ile iliyodhihiri duniani kwa madai maalumu ya Tauhidi na kushika njia ya wastani hali yake ya kupita mipaka imefikia kiasi hiki, basi tusikitikieje mataifa mengine na kuyataja!

Makao Makuu ya Wakristo ni ardhi ambamo busara na nguvu nzuri za ubongo zilitarajisha sana, lakini kwa masikitiko twalazimika kusema kwamba kuhusiana na dini na Tauhidi, hao pia baada ya kusoma sayansi na falsafa walizipoteza. Tunapoona upande mmoja kwamba wameshafika kileleni katika tadbiri ya mambo

ya dunia na utaratibu wake na kuunda viwanda vya kisasa, na kisha tuonapo upande wa pili kwamba wameshaanguka vibaya namna gani katika suala la kumtambua Mungu na wamemfanyaje mtu mmoja mnyonge kuwa Mola wa walimwengu, tunashangaa kwamba katika mambo ya dunia busara yenye ustadi kiasi hiki, na katika kumtambua Mungu akili na welekevu haba kiasi hiki! Na tuchunguzapo kwa makini kwamba kuna sifa bainishi gani kati ya Wakristo na Waislamu juu ya kuzidisha na kupunguza kupindukia, yaonekana kwamba miongoni mwa Waislamu wako wengi wanaonyima haki za wanadamu, na miongoni mwa Wakristo wako wengi ambao wananyima haki za Mungu. Kwani, kosa la suala la jihadi limezifanya nyoyo za Waislamu kiasi hiki kwamba ndani ya mioyo yao haikubaki huba ya kweli ya wanadamu. Kwa hiyo, watu katili miongoni mwao, kwa matamanio duni ya nafsi au kwa jazba ya kishetani wanakuwa tayari kumwua mtu asiye na hatia, wala hawaogopi kumfedhehesha na kunyang'anya mali, na wakipoteza sehemu muhimu ya haki za wanadamu wametia doa baya katika ubinadamu. Kisha tukiona kwa makini hali za Wakristo, basi inadhihirika waziwazi kwamba walifanya kila liwezekanalo kunyima haki za Mungu na wakamfanya mtu mnyonge kuwa Mungu bila sababu yoyote. Na kwa lengo ambalo walimfanya Mungu, lengo lile pia hawakulipata. Kama kwa kuepukana na dhambi, dawa ilikuwa kuamini tu damu ya Yesu Masihi, basi kwa nini

dawa hiyo haikuweza kuwatakasa watu wa Ulaya katika dhambi ya kuiabudu dunia na dhambi ya matamanio haramu ya aina aina ambayo hata kuyataja pia ni aibu, bali kinyume chake imezidi zaidi ya kawaida. Je, nchi za Ulaya ziko nyuma katika maovu kuliko nchi za Asia? Basi, kwa nini haikuchunguzwa upya dawa hiyo isiyo na athari. Kwa ajili ya afya ya siku chache kila daktari na mgonjwa anashikamana na kanuni hii kwamba kama dawa fulani haifaidishi hadi wiki au siku kumi, basi lazima dawa ile inabadilishwa na dawa nzuri zaidi inatafutwa. Kwa sababu gani, basi, juu ya kuthibitika dawa hiyo kuwa si sawa, haijabadilishwa mpaka sasa. Je, baada ya kupita bure miaka elfu moja na mia tisa bado fikira hii inao umuhimu kwamba kuamini damu ya Yesu kunampatia mtu wokovu wa kweli. Au twaweza kutarajia kwamba ingawa mpaka zama hizi dalili bainishi zozote za kuamua hazijadhihirika, lakini katika siku zijazo zama zitawadia kwamba wajikingao na maovu na kunywa chakari watakuwa duniani Wakristo kuliko wengine? Mtu anayeishi katika nchi yoyote ya Ulaya, akitaka anaweza kutoa ushahidi kwamba kauli hii ni kweli, bali kila mwenye akili aliyetembelea Ulaya wakati wowote na akaishi Paris na kadhalika kwa muda fulani, hatasita kushuhudia kwamba sasa baadhi ya sehemu za Ulaya zimefikia hali kwamba inakaribia machoni mwa wengi uzinzi si dhambi tena. Kwao kuoa zaidi ya mke mmoja ni haramu, lakini kutazama wanawake kwa tamaa si haramu. Kwa hakika katika Ufaransa na

penginepo malaki ya wanawake wapo ambao hawana haja ya waume. Basi, twalazimika kusema kwamba kwa ajili yao aya mpya ya Injili imetokeza iliyohalalisha vitendo hivyo vyote, au hakuna budi kusema kwamba dawa ya damu ya Yesu imeathiri kinyume, na dai likawa batili. Lakini, ukweli ni huu kwamba dawa hii haikuwa sahihi, na kifo cha mtu fulani hakihusikani kiasili na wokovu wa mtu mwingine. Na uzima wa Mungu ndio chanzo cha baraka zote, na sio kufa. Na mwanga unapatikana wakati wa macheo ya jua sio machweo. Na kwa kuwa dawa hii haikuweza kutimiza shabaha ya kufutilia mbali dhambi, basi kanuni ile pia haikubaki sahihi kwamba huyo alikuwa mwana wa Mungu ambaye alijiua kwa nia hii. Hatuwezi kukubali kifo cha namna hii kwa Mungu kwamba uzima pia ulipotea na kazi nayo haikufanyika. Kwanza, ni kinyume cha kanuni ya kale ya Mungu kwamba Mungu pia Anaweza kuzaliwa kutoka tumboni mwa mwanamke akikubali mauti na kifo na kila hasara na dhila, kwani dai hili halikuthibitishwa kwa mfano wowote ili ieleweke kwamba mara mbili tatu hapo kabla pia Mungu Alizaliwa kwa njia hii, ili moyo utulie, wala dai hili halikuthibitishwa kwa miujiza ya Mungu iliyo nje ya mipaka ya miujiza ya wanadamu. Kisha juu ya hayo, lengo lenyewe ambalo itikadi hii ilibuniwa kwalo limekosekana kabisa. Kwa kutimiza tamaa za nafsi duniani kuna dhambi mbili kubwa: moja, kunywa pombe na nyingine uzinifu. Sasa semeni, je hii si kweli kwamba wanaume kwa wanawake wa Ulaya,

wengi wao wameshiriki kikamilifu katika dhambi hizi mbili. Bali sitii chumvi nikisema kwamba katika kutumia ulevi, Ulaya imezidi kuliko nchi zote za Asia. Na katika miji mingi ya Ulaya maduka ya kuuza pombe yatakutwa sana hata kwamba maduka ya aina zote ya miji yetu yatakuwa machache sana kulingana nayo. Na uzoefu unashuhudia kwamba mzizi wa dhambi zote ni pombe, kwani katika dakika chache tu ikimlewesha mtu inamjasirisha hata kumwaga damu, na maovu mengine na upujufu ni vitu vyake vya lazima. Nasema kweli kabisa na ninasisitiza kwamba ulevi na uchamungu hauwezi kujumuika. Na mtu asiye na habari ya matokeo yake mabaya, hana busara. Tena kuna shida nyingine kubwa ndani yake kwamba kuacha mazoea haya si kazi ya kila mmoja.

Sasa, kama swali lazuka kwamba kama damu ya Yesu haiwezi kuondolea mbali dhambi – kama vile kwa hakika haikuweza kutakasa – basi, je ipo tiba yoyote ya kuondoa dhambi au la; kwani, maisha machafu kwa kweli ni mabaya zaidi kuliko kufa. Mimi, kwa kujibu swali hili – sio tu kwa madai imara, bali kwa uzoefu wangu na uhakika wa majaribio yangu – nasema kwamba kwa kweli ili kuokoka katika dhambi, tangu mtu alipozaliwa mpaka siku hizi ambazo ni siku za mwisho, njia moja tu imethibitika ya kuepukana na dhambi na maasi, nayo ni hii kwamba mtu kwa hoja ya yakini na kwa ishara zing'aazo afikie maarifa yale yanayoonyesha Mungu kikweli, na inadhihirika wazi

kwamba ghadhabu ya Mungu ni moto unaoteketeza. Kisha kwa onyesho zuri la Mungu, yathibitika kwamba kila ladha kamili imo ndani ya Mungu, yaani kijalali na kijamali mapazia yote yanaondolewa. Hiyo ndiyo njia pekee ambayo kwayo matamanio ya nafsi yanazuilika na kwa vyovyote mabadiliko huzalika ndani mwa mtu. Wakati wa jibu hili wengi watasema, je hatumwamini Mungu? Je hatumuogopi Mungu na hatumpendi? Na je dunia nzima haimwamini Mungu isipokuwa watu wachache? Hao nao wanatenda dhambi ya aina aina na wanaonekana wakifanya upujufu na maasi ya namna namna. Basi jibu lake ni hili kwamba imani ni kitu tofauti na maarifa [ya Mungu] ni kitu kingine. Na lengo la maelezo yetu sio kwamba mumini anaepukana na dhambi, bali lengo lenyewe ni kwamba mwenye maarifa kamili ya Mungu anaepukana na dhambi, yaani yule aliyeonja ladha ya hofu ya Mungu pia na ladha ya huba ya Mungu vilevile. Pengine mtu atasema kwamba shetani anayo maarifa kamili basi kwa nini yu mwasi? Jibu lake ni hili tu kwamba yeye hana maarifa kamili asilani wanayopewa waliobarikiwa. Ni katika asili ya mtu kwamba hana budi kuathirika na elimu ya daraja kamili, na njia ya maangamio inapoonyesha uso wake wa kutisha, yeye haukabili. Lakini uhakika wa imani ni kwamba aamini akiwa na dhana njema; lakini uhakika wa maarifa ni kwamba alione pia aliloamini. Hivyo, ni muhali kujumuika maarifa na uasi ndani mwa moyo

mmoja kama ambavyo ni muhali kujumuika kwa mchana na usiku katika wakati mmoja.

Ni uzoefu wenu wa kila siku kwamba kitu kinapothibitia kuwa na manufaa, mara moja upendo wake huzalika moyoni; na kinapothibitika kuleta madhara, mara moja moyo unaanza kukiogopa. Kwa mfano, asiyejua kwamba kitu kilicho mkononi mwangu ni aseniki, yeye kwa kuifikiria kuwa *tabashir* — Banslochan — au dawa nyingine ifaayo, aweza kuila mpaka tola moja au tola mbili kwa wakati mmoja. Lakini anayejua kwa tajriba yake kwamba hii ni sumu ya kuua, yeye hawezi kuitumia hata kiasi cha gramu moja, kwani anajua kwamba akila tu ataaga dunia. Kadhalika, mtu anapojua kabisa kwamba bila shaka Mungu Yupo, na kwa hakika machoni Mwake dhambi zote zitasababisha adhabu, kama vile wizi, umwagaji damu, uzinifu, dhuluma, uhaini, ushirikina, uongo, kutoa ushahidi wa uongo, kiburi, kujionyesha kwa watu, kula haramu, udanganyifu, kutusi, kudanganya, kuvunja ahadi, kuishi katika mghafala na kulewa, kutomshukuru Mungu, kutomcha Mungu, kutokuwahurumia waja wake, kutomkumbuka Mungu kwa moyo wa kumcha, kuzama kabisa katika anasa na ladha za dunia na kumsahau Mwenye kutuneemesha wa kweli, kutojali dua na unyenyekevu, kuchanganya vitu vibovu katika vitu vinavyouzwa au kupunja, au kupunguza bei kuliko bei ya soko, kutowahudumia wazazi, kutoishi na wake kwa wema, kutomtii mume barabara, kuwatazama wanaume

au wanawake wageni kwa matamanio mabaya, kutojali mayatima, dhaifu, wanyonge, wenye hali ndogo, kutojali kabisa haki za jirani na kumwudhi, kuwafedhehesha wengine kwa kuthibitisha ukubwa wako, kumdhihaki mtu kwa maneno ya kuudhi au kueleza upungufu fulani wa mwili wake kwa kumfedhehesha au kumwita kwa jina baya, au kumtuhumu bila sababu, au kumzushia Mungu uongo, na – Mungu Apishe mbali – kujidai unabii au utume au kujidai kutumwa na Allah, au kukana uwepo wa Mwenyezi Mungu, au kumwasi mfalme mwadilifu, na kuleta uharibifu nchini kwa shari. Dhambi hizi zote, baada ya kujua kwamba kwa kuitenda yoyote katika hizo ataadhibiwa, zinaachika zenyenwe.

Labda mtu akidanganyika aulize swali hili kwamba juu ya kujua pia kwamba Mungu Yupo na kujua pia kwamba adhabu itatolewa kwa kufanya dhambi, hata hivyo tunapata kutenda dhambi, hivyo twahitaji njia nyingine yoyote. Basi tutalijibu lile lile tuliloishatoa mapema kwamba haiyumkiniki asilani wala haiwezekani kwa njia yoyote kwamba mkiishapata maarifa kamili kwamba wakati wa  kutenda dhambi papo kwa papo mtaangukiwa na adhabu kama kupigwa na radi, hata hivyo mtaweza kujasiri kutenda dhambi! Hii ndiyo falsafa ambayo haiwezi kubatilika. Tafakarini, na tafakarini sana, kwamba popote mnapokuwa na yakini kamili kupata adhabu, hapo hamwezi kutenda kinyume cha yakini hiyo. Semeni, je mnaweza kutia mkono wenu ndani ya moto? Je mwaweza kujiangusha chini kutoka

kwenye kilele cha mlima? Je, mwaweza kujitupa kisimani? Je, mwaweza kujilaza mbele ya garimoshi liendalo? Je mwaweza kutika mkono wenu kinywani mwa simba? Je mwaweza kusogeza mguu wenu mbele ya mbwa mwenye kichaa? Je mwaweza kukaa kati mahali inapopiga radi kwa sura ya kutisha? Je hamtoki nje haraka kutoka katika nyumba ambayo boriti yake inakaribika kuvunjika au ardhi inaanza kudidimia chini kwa tetemeko la ardhi? Ebu, ni nani miongoni mwenu ambaye akiona nyoka mwenye sumu kwenye kitanda chake, kisha asiruke hararka chini. Ebu, tajeni jina la mtu ambaye chumba chake alimokuwa amelala kikashikwa na moto, asikimbilie nje akiacha kila kitu? Sasa, semeni, kwa nini mnafanya hivyo na kwa nini mnajitenga na vitu hivyo vinavyodhuru, lakini mambo yaliyo dhambi niliyoyaandika sasa hivi, hamjitengi nayo, sababu yake ni nini? Basi, kumbukeni kwamba jibu analoweza kutoa mwenye busara baada ya kutafakari na kutumia akili ni hili tu kwamba katika hali hizi mbili kuna tofauti ya ujuzi. Yaani, kuhusiana na dhambi za Mungu watu wengi wanao ujuzi mpungufu; wanajua dhambi ni mbaya lakini hawazifahamu kwamba ni kama simba na nyoka. Na ndani kwa ndani wanayo mawazo haya moyoni kwamba adhabu hizi sio za yakini, hata kwamba wanayo shaka katika dhati ya Mungu kwamba Yupo au Hayupo. Na kama Yupo, twajuaje kwamba baada ya kifo, roho itabaki au la; na kama itabaki, twajuaje kwamba kuna adhabu pia ya maasi hayo au

hapana. Bila shaka katika mioyoni mwa wengi mawazo haya mmefichika ambayo hawana habari nayo. Lakini sehemu zote za hofu wanazoziepuka ambazo nimeshaandika tayari mifano yake michache, kuhusiana nazo wote wanayo yakini kwamba kuvikaribia vitu hivyo tutaangamia, kwa hiyo hawavikaribii. Bali, hata kama kwa bahati tu vitu kama hivyo vya kuhilikisha vije mbele yao, huvikimbia wakipiga makelele. Hivyo, uhakika wenyewe ni huu kwamba wakati wa kuviona vitu hivyo, mtu anakuwa na elimu ya yakini kwamba matumizi yao yanasababisha maangamizi. Lakini katika amri za dini hakuna elimu ya yakini, bali ni dhana tu, huku wanatazama kwa macho, na huku kuna kisa tu. Kwa hiyo, kwa visa vitupu dhambi haiwezi kutoweka. Hivyo, nawaambieni kweli kabisa kwamba si Yesu mmoja tu, hata kama ma-Yesu elfu pia wafe msalabani, hawawezi kamwe kuwapatieni wokovu wa kweli. Kwani hofu kamili huondoa dhambi, au huba kamili. Na kwanza kifo cha Yesu msalabani ni uongo wenyewe, kisha hakihusikani hata kidogo na kuzuia jazba ya dhambi. Tafakarini, dai hilo limo gizani ambalo tajriba haiwezi kulishuhudia, wala kitendo cha Yesu kujiua hakihusikani kwa njia yoyote na kusamehewa dhambi za wengine. Falsafa ya wokovu wa kweli ni hii kwamba katika dunia hii hii mtu aokoke katika jahanamu ya dhambi. Lakini tafakarini kwamba je nyinyi mmeokoka katika jahanamu ya dhambi kwa visa kama hivyo, au kwa visa hivyo vya upuuzi ambavyo havina ukweli hata

kidogo na ambavyo havihusiani kwa njia yoyote na wokovu wa kweli, mtu yeyote aliokoka wakati wowote? Tafuteni katika Mashariki na Magharibi; hamtawakuta watu ambao kwa visa hivyo walifikia utakaso wa kweli ambao kwao Mungu Anaonekana, na ambao kwao sio kwamba dhambi inachukiza tu bali ladha za ukweli kwa sura ya Pepo zinaanza, na roho ya mtu ikitiririka kama maji huangukia kizingitini pa Mungu, na kutoka mbinguni nuru moja inashuka na kuondolea mbali giza lote la matamanio ya nafsi. Kadhalika mnapofungua madirisha pande zote nne wakati wa mwangaza wa mchana, mtaona kanuni hii ya asili kwamba mara moja mwanga wa jua utaingia ndani; lakini mkifunga madirisha yenu, mwanga hauwezi kuingia kwenu kwa sababu ya kisa tu fulani. Kwa kupata mwanga mtalazimika kuinuka mahali penu na kufungua madirisha, ndipo mwanga wenyewe utaingia ndani na kuangaza nyumba yenu. Je mtu anaweza kukata kiu kwa kufikiria tu maji? La, hasha! Bali anapaswa kwa kuvumilia kila taabu afikie chemchemi ya maji na aweke midomo yake kwenye maji hayo safi baridi ndipo atatosheka kwa maji yale matamu.

Basi maji ambayo mtatosheka nayo, na uchungu na mchomo wa dhambi utakwisha, ndiyo yakini. Chini ya mbingu hakuna njia yoyote kabisa kwa kujiokoa katika dhambi isipokuwa hiyo tu. Hakuna msalaba wowote uwezao kuwaokoeni katika dhambi. Hakuna damu yoyote iwezayo kuzuia matamanio ya nafsi yenu.

Mambo haya hayahusikani kabisa na wokovu wa kweli. Eleweni mambo ya kweli; tafakarini juu ya mambo ya kweli, na yajaribuni haya pia kama vile mjaribuvyo vitu vya dunia. Ndipo mtafahamu haraka kwamba bila yakini ya kweli hakuna mwanga wowote uwezao kuwaokoeni katika giza la matamanio; na bila maji safi ya busara kamili hakuna kitu kiwezacho kuondoa uchafu wenu wa ndani; na bila kuona utamu wa kweli, uchungu na mchomo wenu hauwezi kamwe kutoweka. Yu mwongo anayewaambieni mbinu mbalimbali, na ni jahili anayetaka kutibu kwa njia nyingine. Watu hao hawawezi kuwapeni mwangaza bali wanawatupeni ndani ya shimo la giza; wala hawawezi kuwapatieni maji matamu, bali wanaongeza zaidi uchungu na mchomo. Hakuna damu yoyote inayoweza kuwafaeni isipokuwa damu ile inayozalika ndani mwenu nyinyi wenyewe kwa maakuli ya yakini; na hakuna msalaba wowote unaoweza kuwaokoeni isipokuwa msalaba wa njia iliyonyoka, yaani kushikamana na ukweli kwa subira. Hivyo, fumbueni macho na kuona kwamba je si kweli kwamba mwaweza kuona tu kwa mwanga si kwa kitu kingine; na mwaweza kufikia makusudio yenu kwa njia tu iliyonyoka, si kwa njia nyingine yoyote. Vitu vya dunia vi karibu nanyi, na vitu vya dini vi mbali. Basi, vilivyo karibu tafakarini juu yao na mfahamu kanuni yao, kisha vilinganisheni na vilivyo mbali, kwani, Yu mmoja tu Aliyeweka kanuni hizi mbili. Ni nani miongoni mwenu awezaye kuona bila macho, au kuweza kusikiliza bila masikio, au kuweza

kusema bila ulimi; kwa nini, basi, hamfaidiki na kanuni hiyo katika mambo ya kiroho. Mkiwa wenye macho, je mnaweza kusimama mahali palipo karibu na shimo refu? Au mkiwa na masikio, je hamwezi kushtuka kwa sauti inayowapasheni habari ya ujio wa wezi? Au mkiwa na ulimi unaowaambieni tofauti kati ya kitu kichungu na kitamu, hata hivyo je mnaweza kula vitu vilivyo vichungu na vyenye sumu vinavyokata ulimi wenu na kuchafua tumbo lenu na kusababisha kutapika na kuvimbisha mwili na hatimaye kuangamiza? Basi, kwa viungo hivyo mwelewe kwamba kwa kiroho pia mnahitaji mpate mwanga mkaone ubaya wa njia zilizo mbaya, na mwipate sauti iwatengayo na njia za wezi na majambazi, na mwipate ladha ili mpate kupambanua baina ya kitu kichungu na kitamu, sumu na kiuasumu. Basi mambo ambayo mnapaswa kuyahitaji kwa kusalimika na maangamio ni haya tu. Haiyumkiniki kamwe kwamba bila kupata mwanga mkiwa kipofu muupate wokovu kwa damu ya mwingine. Wokovu sio kitu kitakachopatikana baada ya dunia hii. Wokovu wa kweli unapatikana katika dunia hii hii. Huo ni mwanga unaoishukia mioyo na kuonyesha ni yapi mashimo ya maangamio. Fuateni njia ya haki na hekima, kwani kwayo mtapata Mungu; na jipatieni harara mioyoni mwenu ili muweze kujisogeza kwenye ukweli. Ni wenye bahati mbaya moyo uliopoa, na ni yenye bahati mbaya tabia ile ihuzunikayo, na imekufa ile dhamiri isiyo na mng'ao. Basi, msipungukiwe kuliko ndoo ile

inayoanguka tupu kisimani na kutoka nje ikajaa; na msijichagulie sifa ya kichujio ambamo maji hayawezi kutulia kabisa na yanakuja kwa njia moja na kutoka kwa njia nyingine. Jaribuni muwe wenye afya na iondoke harara yenye sumu ya homa ya kutafuta mambo ya dunia ambayo kwa sababu yake hamna nuru machoni, wala masikio hayawezi kusikia vizuri, wala ladha ya ulimi si sahihi, wala uwezo katika mikono, wala nguvu katika miguu. Mvunje uhusiano mmoja ili uhusiano mwingine uzalike. Uzuieni moyo usielekee upande mmoja ili moyo upate njia upande wa pili. Mtupieni mdudu mchafu wa ardhi ili mjaaliwe almasi ing'arayo ya mbinguni. Na mwelekee kwenye chanzo chenu – chanzo kile ambapo Adamu alihuishwa kwa roho ya Kiungu, ili mpewe ufalme juu ya vitu vyote kama vile alivyopata baba yenu.

Mchana umeshapita, sasa ni wakati wa Alasiri, inakaribia kuwa saa kumi; usiku upo karibu; jua li karibu kuchwa. Sasa mkitaka kuona, basi oneni; mtaonaje baadaye! Kabla ya kuondoka kwenu tangulizeni vyakula vizuri wala si mawe na matofali. Na pelekeni mavazi ya kuvaa sio miba wala takataka. Mungu Anayetia maziwa matitini kabla ya mtoto kuzaliwa, Ndiye Aliyemtuma mmoja kwa ajili yenu katika zama zenu, ili awanyonyesheni kama mama. Yeye ndiye atakayewanyonyesheni maziwa ya yakini yaliyo meupe zaidi kuliko jua na yenye kufurahisha zaidi kuliko vileo vyote. Hivyo, kama mmezaliwa wazima si wafu, basi

njooni mkakimbilie kwenye ziwa hili, kwani mtakunywa humo maziwa mabichi zaidi, na tupeni maziwa yasiyo mabichi yaliyomo vyomboni mwenu na hewa chafu zimeyavundikisha na vidudu wanatambaa ndani yake msioweza kuwaona. Haya hayawezi kuwanurisheni bali yakiingia tu ndani yataharibu afya, kwani sasa hayo siyo maziwa tena, bali ni sumu. Msiusifu kila weupe, kwani baadhi ya vitu vyeusi ni bora zaidi kuliko baadhi ya vitu vyeupe, kwa vile nyewele nyeusi ni alama ya ujana na nguvu, na nywele nyeupe ni alama ya udhaifu, unyonge na uzee. Kadhalika weupe wa kujionyesha kwa watu na kudhihirisha wema ni bure, mtu wa kawaida mwenye dhambi ni bora kuliko yeye, kwani hafichi dhambi yake kwa udanganyifu, basi nasema kikweli kwamba yu karibu zaidi na msamaha wa Mungu. Msivitegemee vitu ambavyo si vya yakini, ambavyo havina mwanga wa kweli, visivyo na falsafa takatifu ndani yao; hivyo vyote ni njia za maangamizi. Pimeni utashi wenu wa mioyo yenu kwamba inataka kitu gani, na kwa njia ipi yaweza kufahamu kwamba kwa njia hii twaweza kutengana na uovu.

Kuhusu tiba gani dhamiri yao inasema kwamba hii itatutosha. Je moyo wowote unakubali kwamba damu ya Yesu itamwogopesha kutenda dhambi? Bali, uzoefu unashuhudia kwamba inamjasirisha zaidi, kwani aitegemeaye damu ya Yesu anajua kafara ya dhambi yake imeshatolewa tayari. Lakini apewaye elimu ya sumu ya dhambi, yeye hawezi kamwe kutenda dhambi, kwani

humo anaona ataangamia. Basi, ametumwa mmoja kutoka kwa Mungu anayetaka kuwafikishieni elimu ambazo kwazo mioyo yenu ipate kumwona Mungu, na ione sumu ya uovu, ndipo nyinyi wenyewe mtaikimbia dhambi kama mtu anavyomkimbia simba. Basi jukumu la lazima la kijitabu hiki litakuwa hili tu kwamba kisambaze mafundisho yake na ishara zake duniani ili watu wanaotafuta wokovu katika msalaba na damu ya Yesu wapate kuona chemchemi ya wokovu wa kweli. Wokovu wa kweli haumo katika maji ambamo sehemu moja ni maji na sehemu ishirini ni matope na uchafu. Maji ya kutakasa mioyo yanateremka kutoka mbinguni kwa wakati wake. Mto upitao ukijaa tele maji hayo unakuwa mbali sana na matope na maji machafu, na watu wanatumia maji yake safi na mazuri. Lakini mto uliokauka, na maji kiasi kidogo yametulia ndani yake nayo ndiyo yananuka pia, haya hayawezi kubaki mazuri na safi, na matope mengi yanachanganyika humo, na wanyama kadhaa hutabawali na hunya humo. Kadhalika, moyo uliojaaliwa elimu toka kwa Mungu na kujaliwa yakini, ndio mfano wa mto uliojaa tele unaomwagilia mashamba yote, na maji yake safi na baridi yanatuliza mioyo na kuondoa uchungu wa maini, nao huo si safi tu wenyewe, bali husafisha pia, kwani hufundisha hekima na busara inayoondoa kutu ya mioyoni na kumfanya mtu kuichukia dhambi. Lakini moyo ule ufananao na maji kidogo yaliyochanganyika na matope, huo hauwezi kuwafaidisha mahuluku kitu wala

hauwezi hata kujisafisha. Basi, sasa ndio wakati; inukeni mkatafute maji ya yakini, mtayapata; na kwa wingi wa yakini mtiririke kama mto. Mkitakasika na uchafu wa kila shaka na wasiwasi muwe mbali na dhambi. Hayo ni maji yatakayoondoa chapa ya dhambi na yakisafisha ubao wa kifua chenu yatatayarisha kwa chapa ya Kiungu. Hamwezi kufuta herufi za nafsi katika ubao wa roho mpaka mzioshelee mbali kwa maji safi ya yakini. Kusudieni mkapewe uwezo, na tafuteni mkapatiwe, na lainisheni mioyo mkaweze kufahamu mambo haya, kwani haiyumkiniki kwamba moyo mgumu uweze kufahamu mambo ya kweli. Je mwafikiri kwamba bila njia ile ya kuimarika moyoni mwenu adhama ya Mungu na kubainika kwenu jalali ya Mungu Aliye Mzima, na kudhihirika kwenu utawala wake, na kujaa moyo nuru ya yakini, mnaweza kupata kuichukia hasa dhambi kwa njia nyingine yoyote? Hasha! Njia ni moja tu, na Mungu Yu mmoja tu, na kanuni ndiyo moja tu.

(Kutoka kwa Review of Religions, Kiurdu, J. 1, Na.1, uk. 9-30, chapa cha Januari 1902)